**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS -TAMISEMI**

HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA

Namba za simu
Mkuu wa shule 0764-124178
Makamu Mkuu wa Shule 0754-023465
0765-995784

SHULE YA SEKONDARI MRINGA
S.L.P 7188,
ARUSHA

Juni 2023

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi………………………………

S.L.P ……………

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MRINGA HALMASHAURI YA ARUSHA DC MKOA WA ARUSHA MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya …….……

Shule ya Sekondari Mringa ipo umbali wa Kilometa 08 Magharibi mwa Mji wa Arusha Usafiri wa basi kutoka mjini Arusha unapatikana katika kituo cha mabasi madogo (DALADALA) Nauli ni Shilingi 500/=, kwa pikipiki ni shilingi 7,000/= na Shilingi 10,000/= kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14/08/2023 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023.

**2.1 Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**<u>SARE YA SHULE</u>**

i. Mashati meupe mawili (2) ya mikono mirefu na yasiyo na urembo wowote.

ii. Sketi mbili, Rangi ya dark kijivu- Kitambaa namba moja (**Dark Gray**).Urefu wa Sketi usipungue sentimita 10 kutoka kwenye kisigino cha mguu. Sketi fupi **HAITAPOKELEWA.** Marinda Matatu kulia na kushoto,mbele na nyuma Box.

iii. Sweta, Rangi nyeusi isiyo na mistari.

iv. Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba visivyo na visigino virefu.
v. Tai, Rangi nyeusi yenye mistari mieupe.
**vi.** Rangi ya hijab ni nyeupe inayoishia chini ya kifua. (**Kwa waislamu tu**)
**vii.** Aje na pull neck nyeusi kwa aijli ya baridi.

## 2.2 MAHITAJI MENGINE YA SHULE

i. Shamba dress gauni la solo, rangi ya kijivu ndefu sentimeta 10 kutoka kwenye kisigino cha mguu.
ii. Track suit **Dark blue** yenye mistari mweupe.
iii. Bakuli, sahani na kijiko (visiwe vya udongo).
iv. Rimu moja ya karatasi za photocopy na Rim moja ya rulled (mistari).
v. Godoro Ia futi 2 ½ na neti
vi. Shuka mbili rangi ya bluu.
vii. Blanketi moja (1).
viii. Mto wa kulalia.
ix. Nguo za kulalia (Night dress).
x. Sanduku Ia chuma dogo.
xi. Ndoo lita 20, kwa ajili ya usafi.
xii. Madaftari ya kutosha (counter books).
xiii. Scientific calculator na mathematical set. Kwa masomo yanayohitaji vifaa hivyo.

**NB**: **Mavazi:**

- Nguo za **nyumbani haziruhusiwi shuleni**.
- Wanafunzi wote wa shule wanatakiwa muda wote wavae sare za shule (shamba dress baada ya masomo). Hawaruhusiwi kuvaa nguo nyingine tofauti na sare zinazotakiwa. Nguo zote ni lazima ziwe ndefu na mabega yasiwe wazi.

**VITABU:**
Ifuatayo ni orodha ya vitabu vinavyotumika darasani. Mwanafunzi ajitahidi kuwa navyo angalau baadhi.

I. **ECONOMICS**

- Principle of microeconomics by Dr. H.LAHUJA and S. Chand 20th edition.
- Principle of microeconomics by Dr. H.LAHUJA and S. Chand 19th edition.
- Principle of Economics by M.L. JHINGAN 4th edition.

- Macro Economics Theory by MC Vaksh 14th edition.
- Essential of A. level Economics paper 1 & 2 by Ambrose Odhiambo.
- Micro/Macro-Economic Theory. By M. L. Jhingan.
- Basics Economics by Tayebula (Mganda).

II. **MATHEMATICS**

- Essential for A. level pure mathematics form five by Telemu Majigwa.
- Conceptual Advanced Mathematics Form Five. By Mayombya.(Muhimu aje nacho).
- Advanced mathematics Review 1 & 2.

III. **GEOGRAPHY**

- Principles of Physical Geography: By Monk house
- Human and Economic Geography by Morgan.
- Human and Economic Geography paper 2. By T.D.Msabila
- Practical Geography, by Zisti Kamil.
- Comprehensive Approach to physical Geography by T.D Msabila.

IV. **ENGLISH LANGUAGE**

- Advanced Level English, A practical Approach, second edition by Nicholaus Asheli.
- Writing skills. By Kiura.
- Advanced Dictionary of contemporary English.
- Advanced level English. Oxford.

V. **HISTORY BOOKS:**

- History One & Two (New Edition) – Shibital) muhimu kuja navyo
- Contemporary Historical Events

VI. **ACCOUNTANCY BOOKS:**

- Advanced Accountancy Volume 1 by S. N and S. K Mahenshwari.
- Business Accounting 1 & 2 by Frank Wood 11th edition
- Financial Accounting Sixth edition S. N & S. K Mahenshwari.
- Advanced Financial Accounting simplified Volume II by N. A. Sallem
- Fundamental of Advanced Accounting Volume I by Gupta.

VII. **COMMERCE BOOKS:**

- Dina V.
- Masasi V or VI
- Essential commerce.
- Theory & practice of Commerce by Thomas

**N: B** (1) Kila mwanafunzi awe na vitabu vitatu. Tutakagua siku wanaporipoti.
(2) Mwanafunzi anayesoma English language ni lazima awe na dictionary.

1.1 **Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja**

**VIFAA VYA USAFI WA MAZINGIRA**

Wanafunzi wa kidato cha tano wanapaswa kuja na vifaa vya usafi kama ifuatavyo:

1. EGM - fyekeo 1
2. ECA- Reki 1
3. HGE-soft brum 1 na hard brum 1
4. HGL- Jembe lenye mpin

**1.2 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule **BENKI YA NMB ACCOUNT NAMBA 40801200048. JINA LA ACCOUNT NI Mringa sec school self-reliance.** (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip) **LIPA BENKI AU KWA WAKALA WA NMB, HATUPOKEI FEDHA TASLIMU.**

## 2. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;

viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3. Viambatisho na Fomu Muhimu**

Itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

**MRINGA SECONDARY SCHOOL**

**REQUEST FORM FOR MEDICAL EXAMINATIONS**

**FROM. ……………………………………………….**

**………………………………………………**

**DATE……………………………………………….**

**MR. /MRS /MISS………………………………………**

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time student in Secondary school. The examination should include the following categories:-

1. (a) Eye sight (b) Hearing (c) Limbs
   (d) Speech (e) Venereal Diseases (f) Leprosy
   (g) Epilepsy
2. Neurosis
3. Other serious Disease
4. Pregnancy

**MEDICAL CERTIFICATE**

**(To be completed by a Government Medical Officer)**

5. (a) Eye – sight
   (b) Hearing
   (c) Limbs
   (d) Speech
   (e) Venereal Diseases
   (f) Leprosy
   (g) V- Neuroses
   (h) Other serious diseases
   (i) Pregnancy

Date……………………............................…Signature …………………………………

Station ……………………………………… Destination ………………………………

Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

**SHULE YA SEKONDARI MRINGA**

**<u>FOMU YA KUKUBALI NAFASI NA UTII</u>**

Mimi……………………………………………………………………….. . (Jina kamili)
Kidato cha……………………………. mwaka ……………………………………….
Nakubali na naahidi kufuata sheria na Taratibu za shule kama zilivyopangwa. Nikienda kinyume nichukuliwe hatua za nidhamu.

**TAREHE………………………………  ……………………………………………**

**JINA NA SAINI YA MWANAFUNZI**

Mimi mzazi /Mlezi wa ……………………………………………………………….
Nimesoma na kuelewa /kukubaliana na sheria na kanuni za shule. Endapo mtoto wangu atashindwa kufuata hayo yote hatua kali dhidi yake zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo.

**TAREHE …………………………………  …………………………………………**

**JINA NA SAINI YA MZAZI / MLEZI**

**KUMBUKA:** SHULE YETU WASICHANA **<u>HAWASUKI NYWELE</u>** TAFADHALI KUBALIANA NALO KABLA YA KUSAINI FOMU YA KUKUBALI NAFASI ULIYOPEWA YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MRINGA

Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**4.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule …………………………………….**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0764124178**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0754023465 / 0765995784**
- **Mwandamizi Taaluma 0754480095**
- **Mwandamizi Malezi 0784515488**